

SHERIA NA HAKI

Kwa kila Mwananchi

Ifanye haki



Iwe shauku

Toleo Na. 011

Jarida la kila miezi mitatu

Julai - Septemba, 2012

Jaji wa Mahkama ya Kimataifa Atembelea ZLSC na Kupongeza Utendaji Kazi

JAJI wa Mahkama ya Kimataifa (International Court of Justice) Mheshimiwa Abdulqawi Yussuf amekipongeza Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kwa juhudi za kutoa elimu ya sheria, haki za binadamu na kuwasaidia wanyonge bila ya malipo.

"Nimefurahishwa na kazi za Kituo. Fanyeni kazi kwa bidii ili sekta ya sheria isaidie maendeleo ya nchi," alisema Mheshimiwa Jaji Yussuf alipotembelea ZLSC ili kufahamu utendaji kazi wa Kituo.

Alisema sekta ya sheria inagusa nyanja zote za kiuchumi, kijamii na

kiutamaduni na chachu ya maendeleo katika nchi zilizoendelea na zinazoendelea.

Jaji Yussuf ambaye ni mzaliwa wa Somalia, alisema sheria inasaidia kujenga uhusiano baina ya nchi na watu wake. Bila ya kuwepo sheria ili kurekebisha (*regulate*) tabia za binadamu na mahusiano yao ni sawa na kuwepo fujo katika jamii, alisisitiza.

Alisema sheria inajenga uwezo wa kufikiri na kupanga mawazo yanayotokana na misingi ya sheria bila ya kujali tofauti zilizopo katika nchi au tofauti walizonazo watu.

Akizungumza kuhusu Mahkama ya

Kimataifa yenye Makao Makuu yake huko *the Hague*, Uholanzi, Jaji Yussuf alisema imesaidia kutatua mizozo ya nchi mbali mbali katika Bara la Afrika.

Mahkama ya Kimataifa imetatu baadhi ya mizozo katika nchi za Afrika ikiwemo Nigeria na Cameroon Peninsula, Mali na Burkina Faso, Benin na Niger na Namibia na Botswana.

Alisema mzozo wa Tanzania na Malawi kuhusu umiliki wa Ziwa Nyasa unaweza kushughulikiwa na Mahkama ya Kimataifa.

"Kwa kweli Mahkama ya Kimataifa imesaidia kujenga mazingira ya amani

Inaendelea Uk. 3




MHESHIMIWA Jaji wa Mahkama ya Kimataifa ya Haki (International Court of Justice) Abdulqawi Yussuf (katikati aliyevaa miwani) akipiga picha ya pamoja na baadhi ya wanafunzi wa Kitivo cha Sheria Cha Chuo Kikuu, Zanzibar; Tunguu nje ya Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC). Mheshimiwa Jaji alitembelea ZLSC na wanafunzi walikuwa wakihudhuria mafunzo ya vitendo.

YALIYO NDANI

- Wanafunzi 42 Wa Zanzibar University Wafundishwa Kazi ZLSC Uk. 5
- Wito wa Mahkama Uk 6
- Ufafanuzi Wa Ushahidi Wa Mtoto Uk. 14
- Taarifa ya ZLSC kwa Vyombo Vya Habari Kufuatia Kuzama Meli ya Mv Skagit Tarehe 18-07-2012 Uk. 18

Spika Kificho Azindua Mradi Wa Katiba Pemba




SPIKA wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar (BLW) Mheshimiwa Pandu Ameir Kificho amewataka wasaidizi wa sheria '*paralegals*' kutoa elimu ya Mabadiliko ya Katiba katika maeneo yao bila ya kuingiza ushabiki wa siasa.

Akizindua Mradi wa Elimu ya

Inaendelea Uk. 5

SHERIA NA HAKI

Kwa kila Mwananchi



Iwe shauku

Toleo Na. 011

Jarida la kila miezi mitatu

Julai - Septemba, 2012

Sheha na Watoto wake Wafikishwa Mahkamani Pemba kwa Kupiga

SHEHA na watoto wake watatu wamefikishwa Mahkama ya Mwanzo, iliyopo Chake Chake, Pemba kwa madai ya kuhusika katika shambulio la kuumumiza mwili Aley Seif Said, mkaazi wa Furaha, Shehia ya Mvumoni, jimbo la Wawi, Pemba.

Ilidaiwa na upande wa Mashtaka uliongozwa na Polisi kwamba tukio hilo lilitokea Septemba 1, 2012 na washtakiwa walimpiga Bwana Aley na kumsababishia maumivu ya mwili.

Kumbukumbu za jalada la kesi ya uhalifu Namb. 175/2012, zinaonyesha walioshtakiwa na kuhusishwa na shambulio dhidi ya Alley ni Sheha wa Mvumoni Rashid Said na watoto wake Humud Rashid, Abdalla Rashid na Said Rashid.

Washtakiwa wote walikana shtaka hilo na wapo nje kwa dhamana. Kesi hiyo ilikuwa chini ya Hakim wa Mahkama ya Mwanzo, Chake Chake, Bwana Nassor Suleiman.

Upelelezi wa kesi unaendelea na kesi inatarajiwa kutajwa tena Novemba 12, mwaka huu. Tukio hilo liliripotiwa katika Kituo cha Polisi Chake Chake kabla ya kesi kufunguliwa Mahkamani.

Vile vile, Aley aliliripoti tukio hilo katika Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC), Afisi ya Pemba, Septemba 14, 2012, kwa madhumuni ya kupata ushauri wa

Inaendelea Uk. 19



ALEY Seif Said, mkaazi wa Furaha, Shehia ya Mvumoni, jimbo la Wawi, Pemba, anayedai kupigwa na Sheha na watoto wake watatu kwa sababu ya ugomvi wa kifamilia.